# TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI KWENYE MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA, DAR ES SALAAM TAREHE 10 – 11/05/2018

## KAIMU MKURUGENZI

## APRILI, 2018

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI KWENYE MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA, DAR ES SALAAM TAREHE 10 – 11/05/2018**

***Ndugu Mgeni Rasmi ;***

***Mjumbe wa THTU Taifa;***

***Mjumbe wa Kamati Tendaji ya RAAWU Kanda ya Mashariki;***

***Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, TEWW;***

***Wajumbe wa Baraza;***

***Wageni waalikwa;***

***Mabibi na Mabwana.***

**Habari za Asubuhi,**

Awali ya yote namshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha hapa makao makuu ya TEWW – Dar es salaam kwa ajili ya mkutano huu wa tisa wa Baraza la wafanyakazi wa TEWW. Pia, nikushukuru ndugu mgeni rasmi, kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mkutano wa tisa wa Baraza la wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW). Umeacha majukumu mengi na kuamua kujumuika nasi siku hii ya leo. Hii ni heshima kubwa kwetu kama Taasisi na tunasema asante sana na karibu sana TEWW ndugu mgeni rasmi.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Napenda nikujulishe kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuhudhuria mkutano wa Baraza la Wafanyakazi kama mwenyekiti kufuatia aliyekuwa mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi na Mkurugenzi wa TEWW, Dkt. Fidelice Mafumiko kuteuliwa kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuanzia tarehe 03.04.2018. Nitumie nafasi hii kumpongeza na namshukuru sana mtangulizi wangu kwa kuwa na imani nami kwa kunipendekeza nihudumu kama Kaimu Mkurugenzi wa TEWW kuanzia tarehe 04.04.2018. Pia, nawashukuru sana wafanyakazi wote wa TEWW Makao Mkuu na

Mikoani kwa namna ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano katika kipindi hiki kifupi nilichohudumu katika Ofisi ya Mkurugenzi wa TEWW. Ndugu wajumbe wa

Baraza la Wafanyakazi nawaahidi kuwa nitashirikiana nanyi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi pamoja na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Huu ni mkutano wa tisa wa Baraza la wafanyakazi la TEWW baada ya ule wa nane uliofanyika tarehe 8/6/2017 Makao Makuu ya TEWW jijini Dar es Salaam ambapo mimi nilihudhuria kama Naibu Mkurugenzi (Taaluma, Ushauri na Utafiti). Mkutano huu hufanyika kila mwaka mara moja na huwakutanisha wawakilishi wa wafanyakazi wa TEWW, wajumbe kutoka vyama vya wafanyakazi vya RAAWU na THTU pamoja na mjumbe wa THTU Taifa na mjumbe wa Kamati Tendaji ya RAAWU kanda ya Mashariki ambao hualikwa katika mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TEWW. Tunawashukuru wote kwa kuweza kutenga muda wa kuja kushiriki nasi katika mkutano huu muhimu.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Baraza la wafanyakazi ni hitajio muhimu la kisheria linalolenga kuwashirikisha wafanyakazi katika ushauri na usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya TEWW ili kuhakikisha kuwa menejimenti na wafanyakazi tunatambua wajibu na haki pamoja na kuzingatia maadili ya utumishi ili kuleta matokeo ya utendaji kazi yenye tija, staha na upendo. Menejimenti ya TEWW itaendelea kudumisha mikutano ya Baraza la wafanyakazi ili kuongeza ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kutekeleza majukumu yetu kwa ustawi wa Taasisi na wafanyakazi kwa ujumla.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Kama unavyo fahamu, TEWW ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 12 ya mwaka 1975 ili kutekeleza majukumu

mbalimbali yahusuyo elimu ya Watu Wazima nchini. Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la wafanyakazi kuwa, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ilipendekeza kudurusu sheria hii. Kwa sasa, andiko la vipengele vilivyodurusiwa limewasilishwa kwenye ngazi husika baada ya kuidhinishwa na Bodi ya usimamizi ya TEWW. Maboresho yaliyopendekezwa yanalenga katika kufikia dira ya Taasisi ya kujenga jamii iliyoelimika na inayojiendeleza sawa na kaulimbiu ya TEWW ya "Elimu Haina Mwisho".

Vile vile, Taasisi inafanya tathmini ya Mpango Mkakati wa sasa (2014/2015 – 2018/2019) kwa lengo la kudurusu ili uendane na mahitaji ya sasa ya kujenga Tanzania ya uchumi wa kati inayotegemea uchumi wa viwanda. Hata hivyo kwa sasa, tutaendelea kutumia Mpango Mkakati uliopo hadi hapo tutakapokamilisha kudurusu na kupata Mpango Mkakati mpya (2018/2019 – 2022/2023). Ni mategemeo yangu kuwa Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakufunzi Wakazi na Wakuu wa Kampasi wataendelea kuandaa "OPRAS" zao na kutekeleza majukumu yao kwa kutumia Mpango Mkakati wa sasa.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Ili kuendana na msimamo wa serikali ya awamu ya tano, menejimenti ya TEWW imedhamiria kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Taasisi pamoja na kuhakikisha yanaelekezwa katika kutekeleza malengo ya kipaumbele ya Taasisi kadiri ya mpango kazi wa Taasisi na ule wa Vituo, Kampasi, Idara na Vitengo kwa ujumla. Katika kutekeleza hili, Wakufunzi Wakazi, Wakuu wa Kampasi na Mkuu wa Idara ya Mafunzo wanaagizwa kusimamia ukusanyaji wa ada kwa umakini mkubwa pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wale tu waliolipa ada ndio wanasajiliwa na kupata huduma katika vituo vyote. Pia, tumesambaza barua kwa Wakufunzi Wakazi ili wazifikishe kwa Wadau tuliowasajili kuendesha "Open Schools" ili walipe ada ya uratibu pamoja na kuhakikisha wanafuata taratibu za kuendesha "Open Schoos" kadiri ya miongozo ya TEWW. Kwa upande wetu Taasisi tutaendelea kuboresha huduma zetu kwa wadau ikiwa ni pamoja na kuwatembelea mara kwa mara na kutoa vyeti vya kuhitimu (Leaving Certificates) kwa wakati kuanzia

Novemba, 2018 kwa kutumia mwongozo / mkakati ulioandaliwa na Idara ya Elimu Masafa.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua stadi za kisomo nchini, TEWW imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy) utakaoanza kutekelezwa kuanzia Julai, 2018. Kupitia Mkakati huu, Taasisi itafungua vituo vya kisomo katika mikoa 21 ya Tanzania bara ili kutoa fursa kwa vijana na watu wazima ili wapate fursa ya kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na kupata stadi za ujasiriamali na ufundi unaoendana na mazingira yao. Ili kufanikisha lengo hili, TEWW itatumia wanafunzi wetu wanaosoma Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Taasisi zilizopo WAMO - Morogoro, Dar es salaam na Luchelele - Mwanza pamoja na vijana wa kujitolea (volunteers) ambao watapatiwa mafunzo maalumu. Wito wetu kwa jamii ni kujitokeza ili kutumia fursa hii ya kisomo na wale wanaopenda kujitolea katika vituo vyetu wawasiliane na Wakufunzi Wakazi katika mkoa husika.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Katika kuboresha utoaji wa mafunzom TEWW imedhamiria kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kutoa mafunzo na uendeshaji wa Taasisi. TEWW imekamilisha uwekaji wa mtandao wa intaneti (LAN) Makao Makuu kwa kushirikiana na Mtandao wa Tafiti za Kielimu Tanzania (TERNET) ili kuimarisha mawasiliano na mafunzo kwa njia ya ujifunzaji huria na masafa (ODL) pamoja na ujifunzaji wa kawaida (regular mode) katika Kampasi ya Dar es salaam, Luchelele – Mwanza na WAMO – Morogoro na vituo vyetu vyote. Vile vile, Taasisi itaboresha maktaba ya Makao Makuu ili vitabu na machapisho mbalimbali yaweze kutumika na wanafunzi wetu wote waliopo nje ya Dar es salaam.

**Ndugu Mgeni Rasmi;**

Mwisho kabisa, sina budi kukiri kuwa mafanikio haya yote na mengine mengi tuliyo fikia ni matokeo ya kazi nzuri inayotokana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya menejimenti na wafanyakazi wote, vyama vya wafanyakazi na Baraza la Wafanyakazi la TEWW ambalo hutoa ushauri kwa Menejimenti. Aidha mafanikio haya huenda yangekuwa makubwa na mengi zaidi kama siyo changamoto mbalimbali zinazotukabili zikiwamo ukosefu wa ofisi za kudumu katika baadhi ya mikoa, upungufu wa wafanyakazi kutokana na kustaafu na vifo na vilevile upungufu wa fedha za ndani. Mwisho kabisa, naomba nikukaribishe rasmi sasa uweze kufungua mkutano wa tisa wa Baraza la Wafanyakazi la TEWW wa mwaka 2018.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.**